

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE

TAARIFA YA MAKABIDHIANO YA PIKIPIKI KWA WATAALAMU WA MIFUGO MWAKA 2017

1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze kupitia Idara ya Mifugo na Uvuvi ilitenga kiasi cha **Tsh. 22,500,000/=** kwa ajili ya ununuzi wa pikipiki **10** kwa ajili ya maafisa Ugani wa Mifugo. Ununuzi wa pikipiki hizo ulilenga kufanikisha huduma za ugani ili mifugo pamoja na wafugaji waweze kufikiwa kwa urahisi na kupatiwa huduma kwa wakati. Aidha pikipiki hizo ni awamu ya kwanza tu na awamu ijayo wataalamu waliobaki nao watapatiwa usafiri ili waweze kuhudumia jamii na kuleta ufugaji wenye tija. Mheshimiwa Mbunge, Makamo Mweyekiti wa Halmashauri, Wataalamu wa Halmashauri pamoja na Waandishi wa habari walihudhuria katika makabidhiano hayo. Iwani wakiwa kama wakulima na wafugaji, wataalamu wa kilimo na mifugo, wakulima na wafugaji, maafisa Tarafa na baadhi ya maafisa watendaji wa Kata walihudhuria katika maonesho hayo.

2.0 MAKABIDHIANO YALIVYOFANYIKA

2.1 UTAMBULISHO

Afisa Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri aliwatambulisha maafisa ugani wote waliowasili kwa ajili ya makabidhiano ya pikipiki kwa Mgeni Rasmi Mh. Ridhiwani Kikwete .

2.2 TAARIFA FUPI YA MAKABIDHIANO YA PIKIPIKI KWA MGENI RASMI

Taarifa fupi ilisomwa kwa Mgeni Rasmi ikielezea takwimu ya mifugo yote ya Halmashauri ya Chalinze, Idadi ya maafisa ugani waliopo, Idadi ya pikipiki zilizokuwepo awali na idadi ya pikipiki mpya zilizonunuliwa. Aidha gharama zilizotumika katika ununuzi wa pikipiki pia zilainishwa kwenye taarifa. Maafisa

Ugani waliokabidhiwa pikipiki watasaini mkataba wa makubaliano na mwajiri wake na atachangia asilimia 50 ambayo ni sawa na Tshs. 1,125,000 tu.

2.3 NENO LA MAKAMO MWENYEKITI KWA MAAFISA UGANI

Mh. Mbode

Makamo Mwenyekiti alishukuru Halmashauri kwa kufata maagizo mbalimbali yanayokuwa yakitolewa kwenye vikao likiwemo la ununuzi wa pikipiki kwa maafisa ugani. Aliwataka Maafisa Ugani watunze vyombo vya usafiri kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wanaohitaji huduma za mifugo. Maafisa Ugani walishauriwa kufanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa pikipiki hizo zinatunzwa na kufanyiwa service pale mda unapofika.

2.4 NENO LA MGENI RASMI MH. RIDHIWANI KIKWETE

Mgeni Rasmi Mh. Ridhiwani Kikwete alizungumza yafuatayo;

- Mh. Aliwashukuru watendaji wa Halmashauri kwa kutii maagizo mbalimbali ambayo hua yanatolewa
- Alizungumzia juu ya migogoro ya wafugaji na wakulima na kuwataka Maafisa waacha visingizio vya kukosa vitendea kazi.
- Pikipiki hizo zisaidie katika kusambaza chanjo za mifugo vijijini.
- Vitendea kazi hivyo vilenge kazi iliyokusudiwa tu.
- Vyombo hivyo vitumike kufikisha sera ya ufugaji wa kisasa.
- Vyombo hivyo vya usafiri vitumike katika kutoa elimu mbalimbali zinazohusu mifugo.
- Vyombo hivyo vya usafiri vitumike kupiga kampeni ya kupiga chapa ng'ombe ili kuwepo na idadi halisi ya mifugo iliyopigwa chapa katika kila Kata.
- Maafisa ugani wakahimize utunzaji wa mazingira na kutoa elimu ya kuzuia ukataji miti kwa ajili ya ufugaji

- Alimalizia kwa kukumbushia kuwa Mh. J.P Magufuli amesisitiza juu ya ufugaji wa kisasa na utunzaji wa mazingira.

2.5 MAKABIDHIANO YA PIKIPIKI

Mh. Mbunge Ridhiwani Kikwete ambaye ndiye alikuwa Mgeni Rasmi aliwakabidhi pikipiki Maafisa Ugani na jumla ya Pikipiki 10 zilikabidhiwa . Mh. Ridhiwani Kikewte alitoa Lita tano za mafuta kwa pikipiki zote kama kianzio cha kuhamasisha utekelezaji.

2.6 NENO LA SHUKRANI KUTOKA KWA MAAFISA UGANI

Afisa Mifugo wa Kata ya Msata kwa niaba ya Maafisa Ugani wote waliokabidhiwa pikipiki alimshukuru Mgeni Rasmi pamoja na Uongozi wa Halmashauri kwa kwa ujumla na kuahidi kufanya kazi kwa weledi na kwa moyo wote ili kufanikisha utendaji yakinifu katika sekta ya mifugo.

2.7 NENO LA SHUKRANI KUTOKA KWA MKURUGENZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri alisema kuwa hayo yote yamefanyika kwa nia ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa Halmashauri. Pia aliahidi kufanya utaratibu wa kuwanunulia pikipiki Maafisa Watendaji wa Kata. Alisisitiza kuwa Halmashauri ya Chalinze itaongeza katika zoezi la kupiga chapa.

Naomba kuwasilisha.

JULIETH EVANCE

KNY: AFISA MIFUGO NA UVUVI (W)

CHALINZE